KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 17, Issue 4

27th Muharram 1433

23rd Dec, 2011

YALIYOMO

WASIFU WA AL-BAANI 1 - 2

RIFQAN AHLUS SUNNAH 2 - 4

WASIFU WA SHEIKH AL-ALBAANI

NA: DR. 'AASIM 'ABDULLAAH AL-QARYOOTI

Sheikh Muhammad al-Haaj Nooh Najjaatee al-Albaani (رحمه الله) alizaliwa katika mji wa Ashkodera, uliokuwa katika wakati huo ndio mji mkuu wa Albania mwaka wa 1332 H (inayoafikiana na 1914 C.E) kutoka katika jamii ya kimasikini. Babake, al-Haaj Nooh Najjaatee al-Albaani alikamilisha masomo yake ya 'Ilmu ya Sharee'ah mjini Istanbul na akarudi kwao Albania akiwa ni mwanachuoni wa madh-hab ya ki-Hanafee. Baada ya nchi ya Albania kutawaliwa na makafiri wasioamini Mungu, jamii yake yote, chini ya uongozi wa babake, iliamua kuhamisha makaazi yao hadi katika miji ya ki-Islamu. Wakenda kuishi Damascus huko Syria. Alipokuwa huko Damascus, Sheikh Al-Albaani alikamilisha masomo yake ya kimsingi na baadae akasomeshwa Qur'an, Tajweed, utaalamu wa lugha ya kiarabu, somo la fiqh ya madh-hab ya Hanafee na 'ilmu nyengine mbalimbali za dini. Alisoma masomo yote hayo chini ya mashekhe tafauti tafauti wakiwemo marafiki zake babake.

Vilevile alipata wasaa wa kusomea ujuzi wa utengezaji wa saa kutoka kwa babake – ujuzi huo ukampa umaarufu mkubwa mpaka akawa ni mwenye kuendeleza maisha yake kutokana na mapato ya kazi yake hiyo. Sheikh alipendezwa mno na makala yaliyokuwa yakitolewa katika jarida la 'al-Manar', na jambo hilo likamtia hima kwa upande wa masomo, ndio akaanza kutaalamika katika ukumbi wa 'ilmu ya hadeeth na masomo mengine yenye kuhusiana nayo akiwa na umri wa miaka 20.

Akaanza shughuli katika fanni hii kwa kunukuu kitabu kinachostahili kukumbukwa cha 'al-Mughnee an-hamlil -Asfaar fil Asfaar fee takhreej maafil-Ihyaa minal-Akhbaar' kilichoandikwa na al-Haafidh al-'Iraaqee. Nae akaongezea nukta zake katika kukinukuu kitabu hicho.

Akabobea zaidi kwenye bahari ya Hadeeth na vitagaa vyake vya kitaalamu licha ya kuvunjwa moyo na babake. Zaidi ya hayo, hakupata baadhi ya vitabu alivyokuwa akivihitaji katika maktaba ya babake ambayo, kwa hakika ilikuwa na vitabu vya fiqh ya ki-Hanafee. Sasa kwa vile Sheikh hakuwa na uwezo wa kununua vitabu vyingi alivyohitaji na visivyopatikana katika maktaba hiyo ya babake, akaanza kuazima vitabu kutoka katika maktaba mashuhuri ya Damascus – 'al-Maktabatudh-Dhwaahiriyyah' au hata mara nyengine kutoka katika maduka ya wauzaji vitabu.

Alizama kabisa katika utaalamu wa Hadeeth mpaka ikambidi mara nyengine awe akifunga duka lake (la shughuli za kutengeneza saa), na abakie kwenye maktaba bila ya kuondoka kwa muda wa hadi masaa kumi na mbili – akikatiza shughuli hiyo kwa ajili ya kwenda kuswali tu – na hakuwa akiondoka kwenda kula, lakini badala yake alikuwa akibeba kumbwe (chakula chepesi) zake kama mbili hivi kila siku.

Hatimae idara ya pale maktaba ikamruhusu na kumpa chumba maalum kwa shughuli zake za ki-masomo na kumkabidhi ufunguo wake maalum wa kuweza kuingia hapo maktaba kabla ya nyakati za ufunguzi za kawaida. Mara kwa mara, Sheikh hubakia kwenye juhudi hizo za uchambuzi wa 'ilmu kuanzia asubuhi na mapema hadi baada ya 'ishaa'. Katika wakati huwo, alifaidi kuandika vitabu vingi sana vyenye manufaa – vingi kiasi cha kwamba hadi leo kuna ambavyo havijachapishwa.

Usomaji wa Sheikh al-Albaani wa hili somo la hadeeth za Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) ulimsaidia sana yeye mwenyewe na kumuathiri na hatimae kumfanya ageuze msimamo wake na kujiepusha na kufuata ki-Upofu madh-hab yake ya awali, na badala yake kukubali na kuandama Qur'an na Sunnah – kulingana na ufahamu wa watu wema waliotutangulia (As-Salafus Saalih). Kwa kawaida, jambo hili linamaanisha yakwamba mara nyengine alikuwa akitafautiana na baadhi ya mashekhe wa pale mjini ambao waliokuwa wakiandama ki-Upofu madh-hab ya ki-Hanafee, na vilevile maimamu wa ki-Soofee na wazushi wa hapo mjini walioanza kumpinga na kuwachochea watu wa kawaida kwa kumbandika jina la "Mpotofu wa ki-Wahhaabi". Hata hivyo, Sheikh alipewa moyo na baadhi ya mashekhe waheshimiwa wa Damascus aendelee, miongoni mwao ni Sheikh Bahjatul Baijaar, Imaam – Sheikh 'Abdul-Fattaah, na Tawfeeq al-Barzah (رحمه الله)

Kwahivyo, Sheikh alipambana na upinzani mkubwa sana katika juhudi zake za ulinganizi wa Tawheed na Sunnah lakini alijitweka hayo kwa kuvumilia na kusubiri.

Baada ya muda akaanza kutoa Darsa mara mbili kwa wiki na kuhudhuriwa na wanafunzi na waalimu wa chuo-kikuu – ambapo alifundisha vitabu mbalimbali vya 'Aqeedah, Fiqh, Usool na utaalamu wa Hadeeth.

Pia Sheikh al-Albaani akaanza kutayarisha na kupanga misafara ya ki -Da'wah katika sehemu mbalimbali za miji ya Syria pamoja na Jordan.

Baada ya idadi kadhaa ya vitabu vyake kuchapishwa na kuonekana, Sheikh alichaguliwa kufundisha Hadeeth katika Chuo kikuu kipya kilichoko al-Madeenah, Saudi Arabia, kwa muda wa miaka mitatu kuanzia 1381H hadi 1383H – ambapo nae pia alikuwa ni miongoni mwa wahusika wa kamati ya Chuo kikuu.

Baadae, Sheikh akarudia tena masomo na shughuli zake za awali katika 'al-Maktabatudh-Dhwaahiriyyah' na huku akamkabidhi duka lake la saa mmojawapo wa nduguze ili aliendeleze.

Aliwahi kufanya ziara katika nchi mbalimbali kwa malengo ya Da'wah na kuandaa ma-Darsa – pakiwemo miongoni mwa nchi, kama vile Qatar, Egypt (Misri), Kuwait, Emirates (U.A.E), Spain na England (Uingereza).
Alilazimika kuhama mara chungu nzima kwa kusafiri kutoka Syria hadi Jordan, kisha Syria tena, kisha Beirut, kisha Emirates (U.A.E), kisha tena akarudi'Ammaan, Jordan, ambapo ndipo alipovuta pumzi zake za mwisho mnamo 1420H (sawa na Oct 1999C.E) na kuaga Dunia (رحمه الله)
Vitabu alivyowahi kuandika – khaswa kwenye ukumbi wa Hadeeth na utaalamu wake ni zaidi ya 100.
Wanafunzi wake ni wengi wakiwemo miongoni mwao ma-Shekhe wakubwa hivi sasa katika Ulimwengu, nao ni: Sheikh Hamdee 'Abdul-MaJed as-Salafee, Sheikh Muhammad 'Eed 'Abbaasee, Dr. 'Umar Sulaimaan al-Ashqar, Sheikh Mash-hoor Hasan Salmaan, Sheikh Muqbil ibn Haadee al-Waadi'ee (رحمه الله) Sheikh 'Alee Khushshaan, Sheikh Muhammad Jameel Zainoo, Sheikh 'Abdur-Rahmaan 'Abdus-Samad, Sheikh 'Alee Hassan 'Abdul-Hameed al-Halabee, Sheikh Saleem ibn 'Eid al-Hilaalee, Sheikh Muhammad Musa Nasr Aal-Nasr, Sheikh Abdul-Adheem Badawi.

MSIMAMO WA AHLU-S-SUNNAH KUMUHUSU MWANACHUONI PINDI ANAPOKOSEA NI KWAMBA ANAPEWA UDHURU. KWAHIYO, HAFANYWI KUWA NI MZUSHI WALA HASUSIWI.

Na: Sheikh 'Abdulmuhsin al-'Abbaad

Sifa ya kutakasika (kutokuwa na madhambi) si ya mtu yoyote baada ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwahiyo hasalimiki Mwanachuoni kutokana na makosa. Na yoyote mwenye kukosea haandamizwi katika makosa yake, na pia makosa hayafai kuchukuliwa kuwa ndio sababu ya kuaibishwa na kutahadharishwa. Bali, makosa yake machache yasamehewe kwa sababu ya [mambo yake] mengi [yaliyo] mazuri. Yoyote aliyekuwa miongoni mwa wanavyuoni hawa waliotangulia, basi watu na wafaidike kutokamana na ilimu zao pamoja na kutahadhari katika kuwafuata kwenye makosa, na kuwaombea du'aa' na kuwaombea [Allaah] Awarehemu. Na yoyote aliye hai, sawa akiwa ni mwanachuoni au ni Mwanafunzi wa 'ilmu, anastahiki kutanabahishwa kuhusiana na makosa yake kwa upole na ulaini, na kumpendelea usalama wake kutokamana na makosa na kuregea kwenye usawa.

Imaam al-Baihaqee, an-Nawawee, na Ibn Hajar al-Asqalaani ni miongoni mwa Wanavyuoni waliotangulia wakiwa na kasoro katika mas'ala ya 'Aqeedah, na Wanavyuoni pamoja na Wanafunzi wa 'ilmu hawawezi kufanya lolote bila ya usaidizi wa 'ilmu yao – Bali, kwa hakika maandishi yao ni katika marejeo muhimu sana kwa wale wenye kujishughulisha nafsi zao na mas'ala ya ki-ilimu.

Amma kumuhusu Imaam Ahmad bin Husain Abu Bakr al-Baihaqee, basi kwa hakika, katika *as-Siyar* (18/163 na yaliyokuja baada yake), kumuhusu yeye, Imaam adh-Dhahabi amesema, "Yeye ni Haafidh, ni 'allaamah, ni Thaabit, ni faqeeh, ni Sheikh-ul-Islaam. Akasema: "Alibarikiwa katika 'Ilmu yake na aliandika vitabu vyenye faida." Akasema: "Alitoweka ndani ya mji wake akikabiliana na kukusanya na kuandika. Akaishughulikia *Sunan al-Kubraa* katika juzuu Kumi, na hakuna yoyote mfano wake." Ametaja yakuwa ana vitabu vyengine vingi na kitabu chake *as-Sunan al-Kubraa* kilichapishwa katika juzuu kumi Kubwa. Akanukuu kutoka kwa al-Haafidh 'Abdul-Ghaafir bin Ismaa'eel [ambae] aliyesema kumuhusu yeye, "Maandishi yake yamekurubia juzuu elfu moja, ambazo hakuna yoyote aliyemtangulia kwa hilo. Alikusanya baina ya 'Ilmu ya Hadeeth, na Fiqh, Ubainifu wa kasoro za Hadeeth, na upande wa kujumuisha baina ya Ahaadeeth. Adh-Dhahabi pia akasema tena, "kwahivyo, vitabu vya al-Baihaqee ni vyenye thamani kubwa, na faida maridhawa. Ni wachache walioboresha mitungo yao mfano wa Imaam Abi Bakr, kwahiyo ni muhimu kwa mwanachuoni ayazingatie mambo haya, hususan kitabu chake cha *Sunan al-Kubraa."*

Amma kwa Imaam Yahyaa bin Sharaf an-Nawawee, basi katika *Tadhkirah al-Huffaadh* (4/359), kumuhusu yeye, amesema adh-Dhahabi, "Ni Imaam, ni Haafidh, ni mteule, ni Mfano, ni Sheikh-ul-Islaam, nyota wa Mawalii ... muandishi wa vitabu vyenye faida." Amesema, "Pamoja na msimamo alokuwa nao wa kupambana na nafsi yake, na kuwajibika na Ucha-Mungu na kuitakasa nafsi yake na kijichunga,na kuitakasa nafsi kutokamana na kasoro na kuiepusha kutoka kwenye mwelekeo wake. Alikuwa ni Haafidh kwenye Hadeeth, na utaalamu wake, na watu wake, na uswaheeh wake na ila zake; [alikuwa ni] kiongozi kwa 'Ilmu ya ujuzi wa madh-hab."

Na akasema Ibn Katheer katika al-Bidayah wan-Nihaayah (17/540):

Kisha akatilia umuhimu mkubwa katika kutunga na akakusanya vitu vingi. Miongoni mwayo ni yale aliyoyakamilisha na miongoni mwayo ni yale ambayo hakuyakamilisha. Kutokamana na aliyoyakamilisha ni Sharh Muslim, ar-Rawdhah, al-Minhaaj, ar-Riyaadh, al-Adh-Kaar, at-Tibyaan, Tahreer at-Tanbeeh na usahihishaji wake, Tahdheeb al-Asmaa' wal-Lughaat, Tabaqaat al-Fuqahaa, na mengine yasiyokuwa hayo. Kutokamana na ambayo hakukamilisha ni – na iwapo ilikamilishwa, basi haitokuwa na yenye kufanana nayo katika mlango wake –- ni Sherhe ya *al-Muhadh-dhab*, aliyoiita *al-Majmoo'*. Alifika kwenye mlango wa Riba wa kitabu hicho, akatia fora kwa umahiri wake na akakitimiza kikamilifu na kukifanya ni chenye kufaidisha, na akauimarisha ukosoaji wake. Akaweka tahariri yake katika fiqh ya madh-hab [ya Shaafi'ee] na [madh-hab] nyenginezo. Akaandika tahariri katika hadeeth kulingana na inavyostahiki, [maneno yaliyo] mageni, lugha na mambo muhimu yasopatikana isipokuwa hapo ... wala mimi sijui vitabu vya fiqh vilivyo bora kuliko hivyo; pamoja na kwamba ni vyenye kuhitaji mambo mengi ya nyongeza na mategemezi.

Pamoja na ukunjufu wake mkubwa na ustadi kwenye kuandika, hakuwa ni miongoni mwa walioishi sana, kwani muda wa maisha yake ulikuwa ni miaka arubaini na tano; alizaliwa katika mwaka wa 631H na akafa katika mwaka wa 676H.

Ama al-Haafidh Ahmad bin 'Ali bin Hajar al-'Asqalaani, basi yeye alikuwa ni Imaam mashuhuri kutokana na maandishi yake mengi sana. Miongoni mwa maandishi yake muhimu zaidi ni *Fat-h al-Baari Sharh Swaheeh al-Bukhaari*, ambacho ni kitabu kikubwa cha marejeo kwa Wanavyuoni.

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

[Vilevile] miongoni mwao ni *al-Iswaabah*, *Tahdheeb at-Tahdheeb* na *Taqreeb* chake, *Lisaan al-Meezaan*, *Ta'jeel al-Manfa'ah*, *Bulugh al-Maraam* na vyenginevyo.

Na miongoni mwa Wanavyuoni ni al -'Allaamah, mwanachuoni wa Hadeeth, Sheikh Muhammad Naasir ud-Deen al-Albaani. Simjui mwenye kulingana nae katika zama zetu hizi kuhusiana na uangalifu wa mazingatio juu ya Hadeeth na ukunjufu katika kuzifahamu kwake. Hakusalimika na kuteleza kwenye mas'ala yenye kuzingatiwa na wengi kuwa ni makosa kutoka kwake; kama mapendekezo yake kuhusu mas'ala ya hijaab na kusisitiza kwake yakwamba kuufunika uso wa mwanamke ni jambo la waajib, lakini ni katika [kitendo cha] mapendekezo. Iwapo aloyasema ni kweli, basi kwa hakika itazingatiwa kuwa katika haki ambayo haina budi kufichwa, kwa sababu ya baadhi ya wanawake wenye kupendezwa na kuvua hijaab zao wakitegemea rai hiyo. Kama ilivyo katika maneno yake, "Kwa hakika, kuweka mikono [miwili] juu ya kifua baada ya ku-rukuu' ni katika uzushi [bid'ah]." Katika kitabu, Namna Ya Swala Ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) ambayo ni mas'ala yenye ikhtilafu. Na vilevile katika maneno yake kwenye Silsilat adh-Dha'eefah (2355), yakwamba kukosa kuondoa kilichozidi konde moja la ndevu ni katika bid'ah *idhaafiyyah* (ya ziyada). Na kama mabavyo alivyokataza dhahabu ya duara kwa wanawake. Na kwa kukataa kwa matamshi yake katika mas'ala haya, kwa hakika sina budi isipokuwa kwa kuyategemea hayo – na naona pia yakwamba wengine hawawezi kufanya lolote bila ya kutumia – vitabu vyake na faida zitokazo hapo. Ni bora yaliyoje maneno ya Imaam Maalik (رحمه الله): "Kitu chochote huchukuliwa au hukataliwa kutoka kwa mtu yoyote isipokuwa mwendani wa kaburi hili," akaashiriya kwenye kaburi la Mtume (صلى الله عليه وسلم). Na haya ni matangazo yatokayo kwa jamaa'ah miongoni mwa Wanavyuoni katika kuyakariri na kubainisha kusamehewa makosa yake mwanachuoni kulingana na mambo [yake] mengi ya sawa [aliyonayo]:

Amesema Sa'eed bin al-Musayyib (k.93H), "Si kwa mwanachuoni, wala [mtu aliye] Sharifu (Mtukufu), wala [mtu] mwema, isipokuwa huwa na makosa. Wema wa mtu yoyote ukiwa ni mwingi kuliko kasoro zake, basi hizo kasoro zake huondoka kwa sababu ya wema wake, kama ambavyo upungufu wa yoyote umemzidia, basi wema wake huondoka. Wengine wamesema, Mwanachuoni hakusalimika na makosa, kwahivyo mwenye kukosea kidogo na akapata katika mengi, basi huyo ni mwanachuoni, na mwenye kupatia katika kidogo na akakosea katika mengi, basi huyo ni Jaahil."

Na akasema 'Abdullaah bin al-Mubaarak (k. 181H), "Ikiwa wema wa mtu umezidi uzani maovu yake, basi usiyataje maovu yake. Na uovu wake ukizidi uzani wa wema wake, basi usiyataje mema yake."

Amesema Imaam Ahmad (k. 241H), "Mfano wa Is-haaq (yaani; Ibn Raahawaih) hajavuka daraja kutoka Khurasaan, hata kama ametukhalifu katika mambo, kwani kwa hakika watu hawawachi kukhalifiana wao kwa wao."

Amesema Abu Haatim Ibn Hibbaan (k. 354H): "'Abdul-Maalik – yaani., Ibn Abee Sulaymaan – alikuwa ni miongoni mwa watu bora wa Kufah na ma-Haafidh wao. Hukmu ya ujumla kwa kila mwenye kuhifadhi na akapokea hadeeth kutoka kwenye hifdhi yake ni kwamba hukosea. Si katika uadilifu kuiwacha hadeeth ya Sheikh wa kisawasawa mwenye uadilifu uliotengenea kwa sababu ya kosa alolifanya katika upokezi wake. Na lau tungelipitia njia hii, kwa hakika ingelilazimisha sisi kuziwacha hadeeth za az-Zuhri, Ibn Juraij, ath-Thawree, na Shu'bah, kwa sababu wao walikuwa ni miongoni mwa watu wa kuhifadhi na usaheeh. Walikuwa wakipokea kutokamana na hifdhi zao na wao hawakuwa katika walioepushwa na makosa kiasi cha kwamba walikuwa hawafanyi makosa kwenye riwaya zao. Bali, tahadhari na lililo aula zaidi katika mfano wake ni kuyakubali yale ambayo aloyapokea [mtu] mwenye kutegemewa katika riwaya na kuwacha yale yenye uhakika wa kuyakosea, maadamu hilo halikuzidi kutoka kwake kiasi cha kwamba izidi uzani wa [yale ambayo] amepatia. Kwani kama ingelikuwa hivyo, wakati huo, kuepukana nayo kunastahiki.

Amesema Sheikh ul-Islaam Ibn Taymiyyah (k. 728H): "Kutokana na yenye kupasa ni kujua yakwamba kikundi chenye kujinasibisha na wale wenye kufuatwa katika misingi ya Dini na [falsafa] ufasaha wa kuzungumza uko kwenye vigawanyo. Miongoni mwao ni [wale] waliopinga Sunnah kwenye misingi mikubwa, na miongoni mwao ni [wale] waliopinga Sunnah kwa yakini kwenye mas'ala yenye kutatanisha.

Yoyote ambae aliyewahi kuwakosoa wengine kutoka kwenye vipote vilivyo mbali kabisa na Sunnah kuliko alivyo yeye, basi huyo husifiwa kuhusiana na alichokikosoa cha upotofu na kusema kilicho cha haki. Huwenda akawa, hatahivyo, amezidisha kupita kiasi katika kukosoa kwake ambamo hukataa baadhi ya ukweli na akazungumza baadhi ya mambo ya urongo. Kwahivyo, huwenda akawa ameukosoa uzushi mkubwa kwa kutumia uzushi ulio na daraja ndogo kuliko huo, na akakosoa upotofu kwa upotofu ulio na daraja ndogo kuliko huo. Na hizi ndizo hali za watu wengi wa [falsafa] ufasaha wa kuzungumza, wenye kujinasibisha na Sunnah na Jamaa'ah.

Na mfano wa hawa iwapo hawakufanya waliyoyazua maneno ambayo kwayo wanawaganwanya Waislamu, wakifanya wasaidizi na maadui, itakuwa ni katika sampuli ya makosa; na Allaah (سبحانه وتعالى) anawaghufiria Waumini makosa yao kwenye mfano kama huo.

Na kwa sababu hii, wengi miongoni mwa ma-Salaf na ma-Imaam wa Taifa [la Waislamu] huingia kwenye mifano hii; wana taarifa walizoweka kwa ajili ya hukmu isiyo na mafungamano (Ijtihaad) [ambayo] inayopinga yaliyothubutu kwenye Kitaab na Sunnah. Kinyume na [wale] wenye kuungana na wenye kukubaliana nao na kuwafanya maadui za wapinzani wao; wanasababisha mgawanyiko miongoni mwa Jamaa'ah ya Waislamu; Wanakata mawasiliano na kuwatangaza wapinzani wao kuwa ni wenye ku'asi, lakini si wale wenye kukubaliana nao katika mas'ala ya Rai na hukmu zisizo na mafungamano (Ijtihaad); Wanahalalisha kuwapiga vita wapinzani wao, lakini sio wale wanaokubaliana nao, kwani [watu] hawa ni miongoni mwa watu wa kufarikiana na ikhtilafu."

Wengi miongoni mwa Mujtahideen kutoka kwa Salaf na Khalaf wamesema na kufanya mambo ambayo ni Bid'ah, haliyakuwa wao walikuwa hawajui yakwamba mambo hayo ni bid'ah, emma kwa sababu ya hadeeth dha'eef walizodhania kuwa ni swaheeh, kwa sababu ya Aya ambazo walizozifahamu yasiyokusudiwa kutoka kwao, au kwa sababu ya Rai waliyoishikilia haliyakuwa Nass' hazikuwafikia kuhusiana na mas'ala. Ikiwa mtu alikuwa ni mchaji mbele ya Mola wake kadiri ya uwezo wake, huyu ataingia kwenye msemo Wake: **"Mola wetu! Usitutese kama**

tukisahau (tukaacha yaliyo mema) au tukikosa (tukafanya mabaya).”

Na katika swaheeh, ni kwamba Allaah amesema: **“Nimefanya hivyo.”**Imaam adh -Dhahab (k. 748H) amesema: “Kisha kwa hakika, iwapo mkubwa miongoni mwa ma-Imaam wa ‘Ilm amepata sehemu kubwa, kuendelea kwake katika haki kulikuwa kukijulikana, ‘ilmu yake ilikuwa ni ya upeo, uwerevu wake umedhihiri, na wema wake, ucha-Mungu wake, na msimamo wake ulitambulika, makosa yake alisamehewa nayo. Ndio, sisi hatumtangazii yeye kuwa amepotoka, tukamtupilia mbali na tukasahau wema wake! Wala hatumuigizi katika bid’ah zake na makosa yake; tunatarajia toba ya kutoka kwake na hayo.”

Pia akasema; “Na lau kama tungelikuwa ni wenye kumpinga Imaam, tukamu’asi na kumsusia, kila afanyapo makosa katika Ijtihaad yake katika baadhi ya mojawapo ya masaa’il yenye makosa [ambayo] ni yenye kusamehewa kwake, kwa hakika, hapana yoyote miongoni mwetu atakae salimika – Si Ibn Nasr, wala si Ibn Mandah, wala si wale walio bora kuliko wao. Uongofu wa watu kwenye Haki ni Allaah na Yeye ndiye Mwenye Kuwarehemu wenye rehma. Kwahivyo tunajilinda kwa Allaah na *hawaa* na jeuri.

Na vilevile akasema: “Lau kama [ingelikuwa] yakwamba sisi tumuangamize na kumu’asi kila mwenye kukosa katika ijtihaad yake – licha yakwamba imani yake ni yenye kukubalika na hamu aliyonayo ya kuipenda haki – kwa hakika, ni wachache [katika wale] kutokana na ma-Imaam watakaosalimika nasi. Twamuomba Allaah awarehemu watu kwa Rehma zake na Upole Wake.”

Vilevile amesema, “Sisi tunaipenda Sunnah na watu wake. Na tunampenda mwanachuoni kulingana na alichonacho cha kujifungamanisha na tabia njema. Wala hatupendi alolizua kwa tafseer yenye kupendeza. Kwa hakika, mazingatio yako kwenye wema mwingi.”

Amesema Ibn al-Qayyim (k. 751H):

“Kuzitambua fadhla za ma-Imaam wa Uislamu, na makadirio yao, na haki zao, na kwamba wema wao, ‘ilmu zao, na unyenyekevu wao kwa Allaah na Mtume wake, hauwajibishi kukubalika kila jambo wasemalo. Lolote linalotokea katika fatwaa zao katika masaa’il ambayo aliyokuja nayo Mtume yalifichikana kwao, kisha wakasema kwa kiwango cha ‘ilmu zao, haliyakuwa haki ikawa kinyume chao, haikuwajibisha kutupilia mbali matamshi yao kikamilifu, kuwapunguza na kuwakashifu. Kwani hizi ncha mbili zisizokuwa za haki zinapinga malengo. Malengo ya njia ni baina yake hizo ncha mbili , kwahiyo hatufanyi madhambi, wala hatukuepushwa na makosa,

Mpaka aliposema: “Na yoyote mwenye ‘ilmu katika Sheriya na ukweli anajua bila ya shaka yakwamba mtu muheshimiwa aliyetanguliza wema na athari njema katika Uislamu; na yeye ni nafasi kuhusiana na Uislamu na watu wake; huwenda ikapatikana kuteleza na kujikwaa kutoka kwake kwa mambo ambayo anaweza kusamehewa – bali, [yeye] atalipwa kutokana na kujitegemea kwake katika kutoa hukmu. Kwahiyo, hairuhusiwi yakwamba afuatiliwe na kuchunguzwa katika mambo hayo, wala haifai yakwamba nafasi yake, uongozi wake, na daraja yake zibatilishwe kutoka kwenye nyoyo za Waislamu.

Ibn Rajab al-Hanbalee (k. 795H) amesema: “Allaah amekataa kuhifadhika na makosa kwenye kitabu chochote isipokuwa Kitaab chake, na [mtu] mwenye uungwana ni [yule] mwenye kuyasamehe makosa machache ya mtu kwa sababu ya mambo yake mengi mazuri aliyopata [kwayo].”

Fataawa:

DAMU ASILIA ZA WANAWAKE

Na Sheikh Muhammad Ibn Saalih al -’Uthaymeen

Kutumia Vizuizi Vya Heidh:

Q1: Ni nini hukmu inayohusiana na matumizi ya tembe za kuzuiya heidh katika mwezi wa Ramadhaan?
Maadamu hakuna madhara katika matumizi yake na maadamu mume ataruhusu jambo hilo, basi inaruhusiwa kutumia tembe hizo. Hatahivyo, nimekuja kugundua yakwamba hatua hii inaweza kumdhuru mwanamke, hususan kama inajulikana yakwamba kutokwa na damu kwa njia ya heidh ni mpango wa kawaida. Kuzuia mfumo huu wa njia asilia huwenda kukazuia madhara fulani kwa mwanamke. Vilevile matumizi ya tembe hizi kunaweza kuathiri udhibiti wa huo mzunguko wa ada ya kila mwezi kisha jambo hilo humtia kwenye shaka na babaiko kuhusu kuswali kwake na iwapo ana uwezo wa kujamiiana na mumewe au laa. Kwa sababu hii na sababu nyengine zenye kuhusiana, mimi siwezi kusema yakwamba matumizi ya tembe hizi ni haramu, lakini mimi binafsi sipendi wala sihimizi. Mimi nasema yakwamba mwanamke na ayakubali yale ambayo Allâh alomuamrisha na awe na mazingatio juu ya jawabu ya Mtume (صلى الله عليه وسلّم) kwa mkewe ‘Aisha alipopata ada yake ya mwezi baada ya kuhirimia kwa ‘Umra. Mtume (صلى الله عليه وسلّم) alimuuliza ‘Aisha: “Labda huwenda ikawa umepata ada yako?”

‘Aisha akamjibu, “Naam.” Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلّم) nae akamwambia: “Kwa hakika hilo ni jambo ambalo Allâh alilowaandikia mabinti wote wa Adam.”
Mwanamke anatakiwa awe na subira akitarajia malipo mema kutoka kwa Allâh. Iwapo hatoweza kutekeleza Swala na kufunga kwa ajili ya heidh yake, mlango utabaki wazi kwake kuzikumbuka na kuzitamka Sifa za Allâh, kutoa sadaka na kuwafanyia watu mema na vitendo kama hivyo ni mambo makubwa ya ‘Ibaada.

NENO LA BUSARA

Na akasema ‘Abdullaah bin al-Mubaarak (k. 181H):

“IKIWA WEMA WA MTU UMEZIDI UZANI MAOVU YAKE, BASI USIYATAJE MAOVU YAKE. NA UOVU WAKE UKIZIDI UZANI WA WEMA WAKE, BASI USIYATAJE MEMA YAKE.”

Siyar A’laam an-Nubalaa’, cha adh-Dhahabi (8/352, Chapa ya kwanza)

TANGAZO

JISAJILI E-MAIL YAKO KWENYE MTANDAO WETU

http://www.qssea.net

KISHA BONYEZA [OK] TUKUTUMIE KHUTBA ZA IJUMAA NA MIHAD-HARA MENGINE KATIKA E-MAIL YAKO.